*Mulika, Na. 44 (1), 138-151*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Ruwaza za Mofimu za Ukanushi katika Vitenzi vya Kianzwani, Kimwali na Kiswahili

*Sauda Uba Juma*[1]

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na44t1.8

**Ikisiri**

Makala haya yanalinganisha mofimu za ukanushi baina ya lugha za Komoro[2] na Kiswahili. Vipengele vinavyohusika katika uchunguzi huo ni mfanano na tofauti za ruwaza za mofimu za ukanushi katika vitenzi vya Kianzwani, Kimwali na Kiswahili. Suala kuu ambalo limetusukuma katika uchunguzi huu linatokana na ukweli kwamba, kuna kutofautiana kwingi kwa mitazamo ya baadhi ya wanazuoni kuhusu uhusiano wa lugha za Komoro na Kiswahili. Wapo wanazuoni wanaozichukulia lugha za Komoro kwamba zina mnasaba na Kiswahili. Hata hivyo, baadhi ya wanazuoni wanadai kwamba lugha hizo hazina uhusiano wowote na Kiswahili. Hivyo, utafiti huu umechunguza ruwaza za mofimu za ukanushi katika vitenzi vya Kianzwani, Kimwali na kuzilinganisha na Kiswahili ili kubaini namna zinavyofanana na kutofautiana. Kwa hakika, kuna vipengele vingine mbalimbali vya kiisimu ambavyo vingeweza kuchunguzwa katika lugha hizo. Hii haina maana kwamba aina hii ya mofimu ni muhimu zaidi kuliko aina zingine. Makala haya ni sehemu ndogo na mahususi ya utafiti wa kiisimu. Data za utafiti uliozaa makala haya zimekusanywa kupitia usomaji wa nyaraka pamoja na usaili. Uchambuzi wa data umeongozwa na Nadharia ya Ulinganishaji wa Mofimu. Matokeo ya uchunguzi yameonesha kwamba Kianzwani, Kimwali na Kiswahili ni lugha zenye mnasaba mmoja na hivyo zinatokana na lugha yenye asili moja. Hii ni kwa sababu ruwaza za mofimu za ukanushi katika lugha hizo zinalingana ingawa baadhi zinatofautiana kidogo na Kiswahili. Hata hivyo, tofauti hizo ni ndogondogo ambazo zimetokana na umbali wa kijiografia uliopo baina ya wazungumzaji wa lugha hizo na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili.

## 1.0 Utangulizi

Utafiti huu unahusisha lugha za asili zinazozungumzwa katika kisiwa cha Komoro ambazo ni Kianzwani na Kimwali. Komoro ni kundi visiwa katika Bahari ya Hindi vilivyopo baina ya Madagaska na Msumbiji. Visiwa hivyo vinapatikana katika Pwani ya Afrika Mashariki na Pwani ya Msumbiji. Kwa mujibu wa Kipacha (2003), visiwa vya Komoro vipo umbali wa kilomita 300 kutoka Pwani ya

[1] Mhadhiri, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Tanzania. Baruapepe: chudam017@gmail.com

[2] Tunaposema lugha za Komoro, tunakusudia zile lugha za asili zinazozungumzwa na wenyeji, ieleweke kwamba pamoja na lugha hizo kuna lugha rasmi zinazozungumzwa nchini humo ambazo ni Kifaransa na Kiarabu.

Kaskazini ya Msumbiji na pia kutoka Kaskazini mwa Madagaska. Visiwa hivyo vinne ambavyo vinaunda Komoro ni Ngazija, Anzwani, Mwali (Moheli) na Mayotte (Maore) (taz. pia Chiraghdin na Mnyampala, 1977). Tafiti kuhusu uchunguzi wa kiisimu wa lugha hizo zimeshafanyika. Mathalani, Omar (1985) alifanya utafiti kuhusu Kingazija na kugusia kidogo vipengele vya kiisimu vya Kianzwani na Kimwali. Katika utafiti wake, amejadili michakato ya kifonolojia ya Kingazija na kufafanua sauti mbalimbali zinazojitokeza katika Kingazija na jinsi inavyohusiana na Kianzwani pamoja na Kimwali. Kwa mfano, anaeleza kwamba lugha ya Kingazija, Kianzwani na Kimwali zina irabu tano (5), kama ilivyo katika lugha nyingine nyingi za Kibantu. Vilevile, anadai kuwa baadhi ya konsonanti za Kingazija, Kianzwani na Kimwali hazina asili ya lugha za Kibantu, bali zina asili ya lugha ya Kiarabu. Mifano ya konsonanti hizo ni [ð], [θ], [x] na [ɤ]. Aidha, mtafiti huyo anabainisha kuwa michakato mingi ya kifonolojia aliyoichunguza katika Kingazija inafanana na ile ya Kiswahili. Anadokeza kuwa huenda Kingazija ikawa miongoni mwa lahaja za Kiswahili. Hata hivyo, mtafiti huyo alipendekeza kufanyika utafiti zaidi na kuchunguza vipengele vingine vya kiisimu katika Kianzwani, Kimwali na Kimaore ili kuthibitisha au kukanusha madai hayo. Utafiti wa Omar una uhusiano na utafiti huu kwa kuwa ulishughulikia kipengele cha kiisimu ambacho ni fonolojia. Hata hivyo, kipengele hicho ni tofauti na kipengele cha kimofolojia ambacho kinahusisha ulinganishi wa ruwaza za mofimu za ukanushi katika Kianzwani, Kimwali na Kiswahili.

Naye Nurse (1989) alichunguza kipengele cha kifonolojia baina ya Kingazija, Kianzwani na Kiswahili. Katika uchunguzi wake alibaini mabadiliko ya sauti katika lugha hizo na kulinganisha na Kiswahili na lahaja zake. Kwa mfano, sauti /t̪/ na /č/ kutoka katika lahaja za Kiswahili, zimejitokeza kama sauti /ts/ katika Kingazija na Kianzwani. Kadhalika, sauti /nd/ na /ɟ/ katika lahaja za Kiswahili zimebadilika na kuwa sauti /dz/ katika Kingazija na Kianzwani. Vilevile, sauti /z/ katika lahaja za Kiswahili zimejitokeza kama /dz/ katika Kingazija na Kianzwani. Kazi za wanazuoni hao zimejikita zaidi katika kushugulikia kipengele cha isimu ambacho kinahusu fonolojia, tofauti na utafiti huu ambao umeshughulikia kipengele cha kimofolojia kinachojikita zaidi katika uchunguzi wa ruwaza za mofimu za ukanushi katika Kiazwani, Kimwali na Kiswahili.

Utafiti mwingine ambao ulishughulikia uchunguzi wa kiisimu ni ule wa Chamanga (2010) ambaye pia alichunguza kipengele cha kifonolojia. Katika utafiti wake, alibainisha konsontanti na miundo mbalimbali ya silabi za Kingazija na Kianzwani ambayo inatokana na konsonanti alizozibainisha. Miundo ya silabi iliyobainishwa na mtafiti huyo, imechukuliwa kama konsonanti halisi za Kingazija na Kianzwani ambazo ni: [mɓ, mb, nɗ, nd, ndj, ndr, ndz, nk, nts, djw, gw, hw, kw, nw, ɓw, bw, fw, mw na pw]. Kwa mtazamo wake, mtafiti huyo aliichukulia miundo hiyo kama konsonanti halisi za Kingazija na Kianzwani ambapo alipata idadi ya konsonanti zaidi ya 50 katika lugha hizo. Hata hivyo, tukiichunguza kwa makini miundo yote

hiyo huenda ikawa siyo konsonanti halisi za lugha hizo, bali inaweza kutambulika kama miundo mbalimbali ya silabi inayotokana na mjengeko wa konsonanti halisi za Kingazija na Kianzwani. Mbali na uchunguzi wa kifonolojia, Chamanga (2017) alichunguza pia kipengele cha kimofolojia katika Kianzwani ambapo alibainisha mofimu zinazojitokeza katika aina mbalimbali za ngeli alizozibainisha. Katika uchunguzi wake, alieleza kuwa Kianzwani kina idadi ya ngeli 16. Mathalani, ngeli ya 1 katika Kianzwani inawakilishwa na mofimu {m}, {mu} na {mw} kama ilivyo katika maneno *muntru/mntru (mtu)* na *mwana (mtoto)*. Katika ngeli ya 2, maumbo hayo ya mofimu yanawakilishwa na mofimu {wa} katika maneno *wantru (watu)* na *wana (watoto)*. Vilevile, alibainisha ngeli ya 3 ambayo inawakilishwa na mofimu {m}, {mu} na {mwa} kama ilivyo katika maneno *mnandzi (mnazi), muji (kijiji)* na *mwaha (mwaka)*. Maneno hayo yanabadilika yanapowekewa mofimu katika ngeli ya 4 ambapo yanachukua mofimu {mi} na {mu}, mathalani, katika maneno *minadzi (minazi)* na *miji (vijiji)*. Pamoja na kwamba tafiti hizi tangulizi zimeshughulikia vipengele vya kiisimu ambavyo ni fonolojia na mofolojia, tafiti zao zinatofautiana na utafiti huu ambao umechunguza ulinganishi wa ruwaza za mofimu za ukanushi katika vitenzi vya Kianzwani na Kimwali ili kubaini namna zinavyofanana na kutofautiana na za Kiswahili.

### 1.1 Mofimu za Ukanushi

Dhana ya mofimu za ukanushi katika lugha ni kipengele cha kiisimu ambacho kimefafanuliwa na wanaisimu mbalimbali. Baadhi yao ni Mgullu (1999), Haspelmath (2002), Bauer (2003), Spencer na Zwicky (2003), Aronoff na Fudeman (2011), Matthews (2014) na Katamba (2017) kwa kuwataja wachache. Katika kazi zao, wanafafanua kuhusu dhana ya mofimu za ukanushi na kujadili jinsi zinavyotumiwa kubadilisha maana ya maneno katika lugha mbalimbali. Mathalani, Bauer (2003) anaeleza kuwa mofimu za ukanushi ni zile zinazotumiwa katika lugha mbalimbali ili kuonesha ukanushi au kutengua maana ya neno au sentensi. Mofimu hizo zinaweza kuongezwa kwenye mizizi ya maneno ili kubadilisha maana yake kuwa hasi au kutengua sifa fulani. Akifafanua zaidi kuhusu mofimu hizo, Bauer anaeleza kwamba mofimu za ukanushi katika Kiswahili mara nyingi huundwa kwa kuongeza mofimu {si} kabla ya neno husika. Kwa mfano, neno *siyo* hutumiwa kuonesha ukanushi na kutengua maana ya neno au sentensi. Aidha, mofimu za ukanushi za Kiswahili zinaweza kuwa za kipande cha neno/silabi moja au neno zima. Kwa mfano, {si} ni mofimu ya ukanushi ya silabi moja, ambayo inatumika inapounganishwa na neno jingine kama ilivyo katika neno *si kweli.* Aidha, *siyo* ni mfano wa mofimu ya ukanushi wa neno zima.

Kwa upande wake Wesana-Chomi (2017) anafafanua kwamba mofimu za ukanushi katika Kiswahili ni zile zinazooneshwa katika kitenzi kanushi, kitenzi ambacho huarifu kutofanyika kwa jambo wakati kitenzi yakinishi huarifu kufanyika kwa jambo kama inavyojidhihirisha katika mfano ufuatao:

**Mfano Na. 1:**

| **Uyakinishi** | **Ukanushi** |
|---|---|
| *mtoto anacheza* | *mtoto **ha**chezi* |
| *watoto wanacheza* | *watoto **ha**wachezi* |
| *mimi ninacheza* | *mimi **si**chezi* |
| *sisi tunacheza* | *sisi **ha**tuchezi* |
| *wewe unacheza* | *wewe **hu**chezi* |
| *nyinyi mnacheza* | *nyinyi **ha**mchezi* |

Tukichunguza data katika Mfano Na. 1 hapo juu, kwa mujibu wa Wesana-Chomi (2017), umbo msingi la mofimu ya ukanushi {ha} lina alomofu tatu. Alomofu hizo hutumiwa katika mazingira tofautitofauti kulingana na nafsi ya mzungumzaji katika neno linalohusishwa na mofimu hizo. Kwa mfano, mofimu ya ukanushi {ha} inahusishwa na mzungumzaji katika nafsi ya 3 umoja na nafsi ya 2 wingi. Kwa ujumla, ulinganishi wa ruwaza za mofimu katika lugha ni njia muhimu ya kuchunguza na kulinganisha vipengele vya mofimu katika lugha tofauti. Kwa msingi huo, utafiti uliozaa makala haya ulichunguza jinsi ruwaza za mofimu za ukanushi zinavyojitokeza katika Kianzwani na Kimwali kwa minajili ya kubaini jinsi zinavyoingiliana au kutofautiana na Kiswahili.

### 1.2 Ulinganishi wa Ruwaza za Mofimu

Kulinganisha ruwaza za mofimu ni mchakato wa kuchambua na kulinganisha muundo, mpangilio na uhusiano wa mofimu katika lugha tofauti (Booij, 2005). Lengo la ulinganishi huo ni kuchunguza mfumo wa vipengele vya mofimu, muundo wa maneno na sheria za lugha kwa ujumla. Tunalinganisha mofimu katika lugha kutokana na sababu zifuatazo: mosi, ulinganishi wa mofimu unatusaidia kugundua muundo wa lugha. Kwa kuchunguza mofimu katika lugha tofauti, tunaweza kubaini muundo wa lugha na kanuni zinazotawala ujenzi wa maneno. Aidha, tunaweza kuchunguza ruwaza, yaani jinsi mofimu za kiini, awali, tamati zinavyojitokeza na namna vipengele hivi vinavyochangia katika maana na muundo wa maneno. Pili, ulinganishi wa ruwaza za mofimu ni sehemu muhimu ya utafiti wa lugha. Kwa kulinganisha mofimu katika lugha tofauti, tunaweza kutambua uhusiano na mifumo ya kisarufi na kihistoria kati ya lugha hizo. Pia, tunaweza kugundua sheria na kanuni za lugha, uhusiano wa lugha na mifumo ya kisarufi. Mifumo ya kisarufi ni ile ambayo inahusu kanuni na sheria za lugha ambazo zinaweka muundo na uhusiano kati ya maneno katika sentensi. Vilevile, ulinganishi wa ruwaza za mofimu ni mfumo ambao unasimamia jinsi maneno yanavyounganishwa ili kuunda sentensi sahihi. Hii inajumuisha kanuni za kisintaksia, kimofolojia, kifonolojia na kisemantiki. Kwa mfano, mifumo ya kisarufi inaonesha jinsi nomino, viwakilishi, vitenzi na maneno mengine yanavyoundwa na kufanya kazi pamoja katika lugha.

Tatu, ulinganishi wa mofimu unakuwa muhimu wakati wa kufanya tafsiri ya lugha. Kwa kuelewa jinsi mofimu zinavyofanya kazi katika lugha mbalimbali, tunaweza kubuni njia sahihi za kutafsiri maneno na ujumbe kutoka lugha moja hadi nyingine. Nne, ulinganishi wa mofimu unaweza kuwa muhimu katika elimu na ufundishaji wa lugha. Kwa kujifunza jinsi ruwaza za mofimu zinavyojitokeza katika lugha tofauti, wajifunzaji wa lugha wanaweza kukabiliana nazo wanapojifunza lugha mpya. Hivyo, kwa mnasaba huo, tunaweza kuimarisha mbinu za ufundishaji wa lugha. Vilevile, tunaweza kuelewa changamoto ambazo wanafunzi wanaweza kukabiliana nazo wanapojifunza lugha mpya na kubuni njia bora za kuwasaidia katika uelewa na matumizi sahihi ya mofimu.

## 2.0 Nadharia ya Utafiti

Nadharia ya Ulinganishaji wa Mofimu *(Comparative Morphology Theory)* imetumika kuchambua data za utafiti uliozaa makala haya. Nadharia hii iliasisiwa na watafiti kadha wa lugha za Kibantu katika miaka ya 1960 na 1970. Mwanaisimu mashuhuri wa nadharia hii ni Greenberg (1966). Mwanaisimu huyo anajulikana zaidi kama mmoja wa waasisi wa Nadharia ya Ulinganishaji wa Mofimu kwa kuwa alikuwa na mchango muhimu katika kuiendeleza Nadharia hiyo. Greenberg alitumia Nadharia ya Ulinganishaji wa Mofimu katika utafiti wake wa lugha mbalimbali za Kibantu. Katika uchunguzi wake huo, alijikita zaidi kulinganisha mifumo ya mofimu katika lugha hizo. Kwa mfano, katika lugha ya Kinyarwanda maneno *umugabo* (mwanamume), *umwana* (mtoto) na *igitabo* (kitabu) yana mofimu *umu*, *gabo* na *igi*. Aidha, Greenberg alibainisha ujitokezaji wa mofimu za ukanushi katika lugha ya Kixhosa kama ifuatavyo: Maneno *akabhalanga* (andika), *akukho* (hakuna mtu) na *hayikho* (hakuna njia). Hivyo, mofimu za ukanushi alizozibainisha katika lugha hiyo ni {a} na {ha}. Wanaisimu wengine walioiendeleza Nadharia ya Ulinganishi wa Mofimu ni pamoja na Rottland (1982), Parmer (1988), Stump (2001) na Trommer (2017). Katika uchunguzi wao, wameonesha umuhimu wa nadharia hiyo katika kulinganisha mifumo ya mofimu za lugha mbalimbali ulimwenguni.

Msingi mkuu wa nadharia hii umejikita katika wazo kwamba lugha zote zina mifumo ya mofimu ambayo inajumuisha ruwaza na kanuni za jinsi mofimu zinavyoundwa na kubadilika. Mofimu hizo, huweza kuonesha kazi mbalimbali kama vile wakati, ukanushi, namna, nafsi na kadhalika. Hivyo, ulinganishaji wa mifumo hiyo, unaweza kusaidia na kugundua tofauti na kufanana kwa mofimu hizo katika lugha zinazolinganishwa. Kiujumla, kwa kufanya uchambuzi wa mifumo ya ruwaza za mofimu katika lugha mbalimbali, nadharia hii inalenga kutoa ufahamu na mifumo ya kulinganisha ili kuelewa tofauti na kufanana kati ya lugha hizo. Pia, inaweza kutumiwa kwa madhumuni ya kulinganisha na kufafanua uhusiano kati ya lugha na kuunda uwezekano wa mifumo ya kawaida na kanuni za jumla za mofimu katika lugha mbalimbali. Hivyo, katika utafiti huu nadharia hiyo imetumika kwa lengo la kulinganisha ruwaza za mofimu za ukanushi baina ya

Kianzwani, Kimwali na Kiswahili ili kubaini namna zinavyolingana na kutofautiana.

## 3.0 Methodolojia

Utafiti uliozaa makala haya ni matokeo ya data za maktabani na uwandani. Chanzo cha data za maktabani kilihusisha upitiaji wa nyaraka mbalimbali kama vile vitabu na tasnifu ili kupata uelewa mpana kuhusu mada iliyohusika katika makala haya. Mtafiti alisoma machapisho mengi ambayo yalimsaidia kuelewa dhana ya mofimu za ukanushi na jinsi zinavyojitokeza katika vitenzi mbalimbali vya Kiswahili katika nyakati tofauti. Data za uwandani zilikusanywa kwa wamilisi wa lugha katika kisiwa cha Anzwani na Mwali, visiwa vidogo vilivyomo ndani ya kisiwa kikuu cha Komoro. Utafiti ulitumia sampuli ya watu 60, kila eneo lilihusisha sampuli ya watu 30. Sampuli hii ilipatikana kupitia mbinu ya usampulishaji nasibu na usampulishaji tajwa. Usaili ndiyo mbinu kuu iliyotumika kupata taarifa kuhusu ruwaza za mofimu za ukanushi katika lugha zilizoshughulikiwa katika utafiti huu. Mtafiti aliandaa maswali ya mwongozo ambayo yalimwezesha kubaini ruwaza za mofimu za ukanushi katika vitenzi zilimojitokeza katika lugha hizo. Mbinu ya usaili ilifanikiwa zaidi kwa sababu mtafiti alishirikiana na watafiti wasaidizi ambao ni wenyeji wa maeneo yaliyohusishwa na utafiti huu. Aidha, utafiti huu ulitumia zana nne katika ukusanyaji wa data. Zana hizo ni kompyuta, kinasasauti, daftari na kalamu. Utafiti ulitumia mkabala wa kitaamuli kwa kuwa data iliyotumika imechambuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo katika kutimiza lengo la makala haya.

## 4.0 Matokeo

Matokeo ya utafiti uliozaa makala haya yamewasilishwa katika vipengele vitatu muhimu: ruwaza za mofimu za ukanushi za wakati uliopo, wakati uliopita na wakati ujao kama ifuatavyo:

### 4.1 Ruwaza za Mofimu za Ukanushi katika Vitenzi vya Wakati Uliopo

Vitenzi vya wakati uliopo ni aina ya vitenzi vinavyotumika kutaja matukio, hali au hali ya sasa. Vitenzi hivi vinatumika kuelezea mambo yanayotokea au yanayofanyika sasa hivi kama mfano ufuatao unavyodhihirisha:

**Mfano Na. 2:**
*(i) Mimi ni**na**kula chakula.*
*(ii) Juma a**na**soma kitabu.*
*(iii) Watoto wa**na**cheza mpira.*
*(iv) Sisi tu**na**kwenda sokoni.*

Katika mfano huo, vitenzi vya wakati uliopo ni *ninakula, anasoma, wanacheza* na *ninakwenda*. Katika vitenzi hivyo, mofimu *na-* iliyotumika inaonesha kwamba kitenzi kinaendelea kutendeka wakati wa kutolewa taarifa. Kwa hakika, si lengo la

makala haya kujadili vitenzi vya wakati uliopo. Hata hivyo, maelezo tunayoyatoa kuhusu vitenzi hivyo ni ya msingi kwa kuwa ufafanuzi wa mofimu tunazozijadili, unaambatanishwa kwenye vitenzi katika nyakati tofautitofauti. Aidha, mjadala kuhusu vitenzi vilivyoshughulikiwa umejikita katika uchunguzi wa ruwaza za mofimu za ukanushi katika Kianzwani, Kimwali na kuzilinganisha na Kiswahili. Data ifuatayo katika Mfano Na. 3 inaonesha ruwaza za mofimu za ukanushi zinavyojitokeza katika vitenzi vya wakati uliopo katika Kianzwani, Kimwali na Kiswahili:

**Mfano Na. 3**

| **Vitenzi vya Wakati Uliopo** | | | **Ukanushi** | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Kiswahili** | **Kianzwani** | **Kimwali** | **Kiswahili** | **Kianzwani** | **Kimwali** |
| *ninakula* | *nsila* | *nsila* | *sili* | *sili* | *sili* |
| *tunakula* | *risila* | *risila* | *hatuli* | *tarisila* | *tarisila* |
| *unaandika* | *usianziha* | *usianziha* | *hatuandiki* | *karisianziha* | *karisianziha* |
| *mnaandika* | *msianziha* | *msianziha* | *hamuandiki* | *kamsianziha* | *kamsianziha* |
| *anaandika* | *asianziha* | *asianziha* | *haandiki* | *kasianziha* | *kasianziha* |
| *wanaandika* | *wasianziha* | *wasianziha* | *hawaandiki* | *kwasianziha* | *kwasianziha* |

Data iliyomo katika Mfano Na. 3 hapo juu inaonesha kwamba, mofimu ya ukanushi ya wakati uliopo katika Kianzwani na Kimwali, nafsi ya kwanza umoja inawakilishwa na mofimu {si} ambayo inalingana na Kiswahili. Mofimu ya ukanushi ya nafsi ya kwanza wingi katika Kianzwani na Kimwali zinawakilishwa na mofimu {ta} ambapo katika Kiswahili inawakilishwa na mofimu {ha}. Aidha, mofimu ya ukanushi katika kitenzi cha wakati uliopo cha nafsi ya pili umoja, Kianzwani na Kimwali zinawakilishwa na mofimu ya ukanushi {ka} ambapo Kiswahili kinawakilishwa na mofimu {hu}. Kwa upande wa nafsi ya pili wingi, Kianzwani na Kimwali zinawakilishwa na mofimu {ka} ambapo katika Kiswahili mofimu hiyo ya ukanushi inawakilishwa na {ha}. Vilevile, katika kitenzi cha nafsi ya tatu wingi kwa wakati uliopo, Kianzwani na Kimwali zinawakilishwa na mofimu ya ukanushi {kwa} wakati Kiswahili kinawakilishwa na mofimu ya ukanushi {ha}.

Mofimu za ukanushi zinajibainisha dhahiri katika vitenzi vya wakati uliopo baina ya Kianzwani, Kimwali na Kiswahili. Aidha, mofimu hizo za ukanushi, zina ruwaza zinazolingana. Hali hii inatokana na ukweli kwamba, tukichunguza mofimu za ukanushi, zilizomo katika Mfano Na. 3 hapo juu, tunabaini kwamba asilimia kubwa zimetanguliwa na mofimu za nafsi mbalimbali. Hata hivyo, pamoja na kwamba mofimu hizo zinajitokeza katika mfuatano unaofanana, baadhi yake zinaonekana kusigana baina ya lugha hizo. Kwa mantiki hiyo, tofauti hizo za mofimu zinazojitokeza, zinadhihirisha kile kinachosemwa na waasisi wa Nadharia ya Ulinganishaji wa Mofimu kwamba lugha zote zina mifumo ya mofimu ambayo inajumuisha kanuni za jinsi mofimu zake zinavyoundwa na kubadilika. Hata hivyo, kanuni hizo zinatofautiana baina ya lugha moja na nyingine. Kutokana na

msingi huo basi, tofauti hizo za mofimu za ukanushi zinazojitokeza katika lugha hizo, zinatokana na ukweli kwamba kila lugha ina umahususi wake katika ujitokezaji wa mofimu mbalimbali kwenye vitenzi vyake tofauti. Hivyo, tofauti hizo zimetokea kwa sababu ya mifumo ya lugha zenyewe.

Zaidi ya hayo, data zilizopo katika Mfano Na. 3 zinaonesha kwamba tofauti za mofimu za ukanushi zinazojitokeza katika data hiyo, zimesababishwa na konsonanti /k/ inayojitokeza katika utamkaji wa vitenzi vya Kiswahili ambapo haijitokezi katika Kianzwani na Kimwali na badala yake inajitokeza konsonanti /h/. Kama ambavyo imeshaelezwa katika kipengele cha 4.1 hapo juu, kwamba, hali hiyo imetokea kwa sababu ya utaratibu wa lugha inayohusika kwa kuwa kila lugha ina mfumo wake wa sauti. Hata hivyo, kwa kawaida lugha zenye chimbuko moja, tofauti ya konsonanti hizo zinachukuliwa kama ni za aina moja, hasa tukizingatia kwamba konsonanti hizo hazipishani sana kiutamkaji na pia zinakaribiana katika mahali pa kuzitamkia. Konsonanti /k/ ni kipasuo hafifu cha kakaa laini na /h/ ni kikwamizi ghuna cha glota. Hivyo, kutokana na hali hiyo, konsonanti hizo /k/ na /h/ zinaweza kubadilishana nafasi kiurahisi katika matamshi.

Kwa mujibu Asiimwe (2019), lugha za Kibantu zimepitia michakato na mabadiliko kadhaa ambayo yameukilia tofauti hizo za konsonanti. Konsonanti /k/ ni kipasuo sighuna cha kakaa laini; katika Kiswahili hujitokeza kama konsonanti /h/, konsonanti ghuna ya glota, katika Kianzwani na Kimwali. Hivyo, tofauti hizo zilizojitokeza zinaashiria mchakato ujulikanao kama ukwamizwaji. Mabadiliko hayo ya konsonanti, yalisababisha konsonanti ya asili kutoka Mame-Bantu /k/ ambayo ni kipasuo sighuna cha kakaa laini kupitia mabadiliko ya kuwa /h/ kikwamizi ghuna cha glota katika mchakato wa ughunishaji. Hivyo, mofimu ya ukanushi {ka} inayojitokeza katika Kiswahili inalingana na mofimu {ha} inayojitokeza katika Kianzwani na Kimwali. Kwa mnasaba huo, hali hii inaonesha kwamba huenda Kianzwani na Kimwali zinatokana na lugha zenye asili moja. Kipengele cha 4.2 kifuatacho kinahusu ruwaza za mofimu za ukanushi zinavyojitokeza katika vitenzi vya wakati uliopita katika Kianzwani, Kimwali na Kiswahili:

### 4.2 Ruwaza za Mofimu za Ukanushi katika Vitenzi vya Wakati Uliopita

Njeo ya wakati uliopita katika Kiswahili hubadilika ikiwa kitenzi ni yakinishi au la. Wakati uliopita katika hali ya ukanushi, kitenzi cha Kiswahili huwakilishwa na mofimu {ku} (Habwe na Karanja, 2012). Tuchunguze Mfano Na. 4 ufuatao katika lugha ya Kiswahili:

**Mfano Na. 4**

| **Wakati Uliopita** | **Kitenzi** | **Neno** |
|---|---|---|
| Yakinifu {**-li-**} | {a+**li**-lim+a} | a**li**lima |
| Kanushi {**-ku-**} | {ha+**ku**+lim+a} | ha**ku**lima |

Habwe na Karanja wanaendelea kueleza kuwa licha ya njeo, kitenzi cha Kiswahili huchukua hali. Hali ni kipegele cha kisarufi ambacho kinatumika katika vitenzi kuonesha muda au kipindi maalumu ambamo tendo limefanyika. Mofimu za hali katika kitenzi cha Kiswahili kwa wakati uliopita hueleza kama kitenzi kimemaliza kufanyika kwa muda au kama kimemaliza kufanyika. Hali hii inawakilishwa na mofimu tofauti za uyakinishi na ukanushi kama ilivyobainishwa katika Mfano Na. 5 hapo chini.

**Mfano Na. 5**

| **Hali Kamilifu** | **Kitenzi** | **Kanushi** | **Kitenzi Yakinifu** | **Neno Kanushi** |
|---|---|---|---|---|
| Yakinifu**{-me-**} | {a+**me**+lim+a} | {ha+**ja**+lim+a} | a**me**lima | ha**ja**lima |
| Yakinifu **{-me-**} | {a+**ka**+chez+a} | {ha+**ku**+chez+a} | a**me**cheza | ha**ku**cheza |

Hivyo, mofimu {me} imetumika katika vitenzi vya wakati uliopita mkamilifu ili kuonesha uyakinishi ambapo mofimu {ja} na {ku} zinaonesha ukanushi wa wakati huo. Hata hivyo, mofimu {ha} inawakilisha ukanushi wa kitenzi katika nafsi ya tatu umoja. Hebu sasa tuchunguze jinsi ruwaza za mofimu za ukanushi zinavyojitokeza katika vitenzi vya Kianzwani na Kimwali katika wakati uliopita kwa kupitia nafsi mbalimbali kama zinavyojidhihirisha katika Mfano Na. 6 hapo chini:

**Mfano Na. 6**

| **Vitenzi vya Wakati Uliopita** | | | **Ukanushi** | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Kiswahili** | **Kianzwani** | **Kimwali** | **Kiswahili** | **Kianzwani** | **Kimwali** |
| *nilipika* | *tsipiha* | *tsipihi* | *sikupika* | *tsapiha* | *tsapiha* |
| *tulipika* | *ripiha* | *ripiha* | *hatukupika* | *karapiha* | *karapiha* |
| *ulipika* | *upiha* | *upiha* | *hukupika* | *kwapiha* | *kwapiha* |
| *mlipika* | *mpiha* | *mpiha* | *hamkupika* | *kamwapiha* | *kamwapiha* |
| *alipika* | *hapiha* | *hapiha* | *hakupika* | *kapiha* | *kapiha* |
| *walipika* | *wapiha* | *wapiha* | *hawakupika* | *kwawapiha* | *kwawapiha* |

Data katika Mfano Na. 6 hapo juu, vilevile imepatikana kutoka uwandani kupitia njia ya usaili. Tukiichunguza data hiyo, tunabaini kwamba Kianzwani na Kimwali zina mofimu za ukanushi za aina mbili. Mofimu hizo ni {ka} na {kwa}, mofimu hizo zinajitokeza katika vitenzi vya wakati uliopita vya nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili umoja na wingi na nafsi ya tatu umoja na wingi. Mathalani, mofimu {ka} inajidhihirisha katika vitenzi vilivyoambatana na nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili wingi na nafsi ya tatu umoja. Vilevile, mofimu {kwa} inajibainisha katika vitenzi vilivyobeba nafsi ya pili wingi na nafsi ya tatu wingi. Hali hii ni tofauti na ujitokezaji wa mofimu za ukanushi katika Kiswahili ambapo {ha} inajidhihirisha katika vitenzi vya wakati uliopita katika nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili wingi na nafsi ya tatu umoja na wingi. Vilevile, katika kitenzi cha nafsi ya kwanza umoja, mofimu ya ukanushi katika Kiswahili imebadilika na

kuwa {hu}. Wakati huohuo, katika kitenzi cha nafsi ya kwanza umoja, mofimu ya ukanushi katika Kianzwani na Kimwali inakuwa {tsa} ambapo katika Kiswahili inakuwa {si}.

Tofauti za mofimu za ukanushi zinazojitokeza katika Kianzwani, Kimwali na Kiswahili zinasadifu barabara msingi wa Nadharia ya Ulinganishaji wa Mofimu iliyotumika katika uchambuzi wa data za utafiti uliozaa makala haya. Msingi mmojawapo wa nadharia hiyo unaeleza kwamba, lugha huweza kuwa na mfumo wa ujitokezaji wa mofimu za kuvunja katika maneno yake mbalimbali. Mofimu hizo zinaweza kutumiwa katika lugha hizo kuunda maneno mapya kutokana na msingi wa maneno ya awali. Kwa mantiki hiyo, kutokana na kulinganisha mifumo hiyo ya uvunjaji wa mofimu, inawezekana kugundua tofauti katika mchakato wa kuvunja maneno katika lugha hizo kama inavyojidhihirisha katika Kianzwani na Kimwali.

Pamoja na tofauti hizo za mofimu zilizojitokeza, ruwaza za mifumo ya mofimu katika vitenzi vya wakati uliopita inalingana kati ya lugha hizo. Mofimu zote hizo za ukanushi, zimejitokeza kabla ya mofimu za nafsi na wakati katika vitenzi hivyo. Vilevile, matokeo ya utafiti yamebaini kwamba kuna mabadiliko ya kifonolojia yanayojitokeza katika baadhi ya vitenzi hivyo. Mathalani, konsonanti [s] katika Kiswahili imebadilika na kuwa [ts] katika Kianzwani na Kimwali. Hii ni kudhihirisha kwamba kuna baadhi ya maneno ya Kianzwani na Kimwali ambapo konsonanti [ts] inatumika badala ya konsonanti [s] inayotumika katika Kiswahili. Hivyo, ni dhahiri kwamba konsonanti hizo zinakaribiana sana kimatamshi na ziko jirani katika mahala pa kuzitamkia. Konsonanti [s] ni kikwamizi cha ufizi na [ts] ni kizuio-kwamizi cha ufizi. Hata hivyo, sauti hizo zina tofauti ya kiumbo na kimatamshi tu, kwani kwa lugha zenye asili moja sauti hizo zinalingana kwa kuwa zinarejeleana. Kuna mabadiliko mengine ya sauti katika mofimu za ukanushi zinazojitokeza katika lugha tunazozizungumzia. Kwa mfano, mofimu ya ukanushi {ha} au {hu} zinapojitokeza katika Kiswahili, badala yake katika Kianzwani na Kimwali zinajitokeza mofimu za ukanushi {ka} au {kwa} badala ya {ha} au {hu}.

Mabadiliko hayo ya kifonolojia, yanaweza kutokea kutokana na utaratibu wa lugha zinazohusika kwa kuwa kila lugha ina mfumo wake wa sauti. Hata hivyo, utafiti uliozaa makala haya unakubaliana na Massamba (2004) anayeeleza kuwa, kwa lugha zenye mnasaba mmoja sauti hizo zinachukuliwa kama ni sauti za aina moja, hasa tukizingatia kwamba sauti hizo hazipishani sana kiutamkaji na pia mahali pa kuzitamkia. Konsonanti [k] ni kipasuo hafifu cha kaakaa laini na [h] ni kikwamizi ghuna cha glota. Hivyo, kutokana na hali hiyo, konsonanti hizo zinaweza kubadilishana nafasi kiurahisi katika matamshi. Aidha, Massamba anaendelea kueleza kuwa mnasaba katika isimu linganishi na isimu historia ni ule upatanifu uliopo baina ya maneno au mitindo iliyo na uhusiano wa kiasili ingawa maumbo

au miundo hiyo inaweza kuwa na sura au maumbo yasiyofanana katika umbo lake la nje.

Anatoa mfano kwa kusema kuwa sauti [ʧ] katika Kiswahili sanifu hugeuka kuwa [t] katika lahaja ya Kimvita. Hivyo, maneno *chini, macho* na *choma* ya Kiswahili sanifu, yanatamkwa *[tini], [matɔ]* na *[tɔma]* katika lahaja ya Kimvita. Kwa mantiki hiyo, sauti [ʧ] na [t] zinarejeana kimnasaba kwa sababu zina upatanifu wa kiumbo licha ya tofauti inayojitokeza. Hivyo, kwa mujibu wa isimu historia na linganishi, Kiswahili na lahaja ya Kimvita ni lugha zinazotokana na lugha yenye asili moja. Kwa mantiki hiyo, konsonanti /t/ na /k/ katika Kiswahili zimebadilika kuwa /ts/ na /h/ katika Kianzwani na Kimwali kama inavyoonekana katika maneno: *[nilipika], [tulipika]* na *[ulipika]* ya Kiswahili ni mnasaba wa maneno *[tsapiha], [karapiha]* na *[kwapiha]* ya Kianzwani na Kimwali. Kwa ujumla, tunaweza kusema kwamba, ujitokezaji wa ruwaza za mofimu za ukanushi za Kianzwani na Kimwali katika vitenzi vya wakati uliopita, unalingana na ule wa Kiswahili. Sehemu ifuatayo inajadili ruwaza za mofimu za ukanushi katika vitenzi vya wakati ujao.

### 4.3 Ruwaza za Mofimu za Ukanushi Zinavyojitokeza katika Vitenzi vya Wakati Ujao

Katika Kiswahili, kuna mofimu za ukanushi zinazotumika katika vitenzi vya wakati ujao. Tuchunguze Mfano Na. 7 ufuatao:

**Mfano Na. 7:**

i. ***Si***takula chakula cha mchana.
ii. ***Ha***takwenda shule kesha.
iii. ***Ha***mtacheza mchezo huo.
iv. ***Hu***taki kuimba wimbo nzuri?

Mifano hiyo inaonesha namna mofimu za ukanushi zinavyoweza kutumika katika vitenzi vya wakati ujao katika Kiswahili. Hata hivyo, matumizi ya mofimu hizo yanaweza kubadilika kulingana na muktadha na aina ya kitenzi kinachotumika. Kwa upande wa Kianzwani na Kimwali, mofimu za ukanushi zinajitokeza kama zinavyoonekana katika Mfano Na. 8 hapo chini:

**Mfano Na. 8**

| **Vitenzi vya Wakati Ujao** | | | **Ukanushi** | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Kiswahili** | **Kianzwani** | **Kimwali** | **Kiswahili** | **Kianzwani** | **Kimwali** |
| *nitakula* | *ntsola* | *ntsola* | *sitakula* | *karitsola* | *karitsola* |
| *tutakula* | *ritsola* | *ripiha* | *hatutakula* | *karitsola* | *karitsola* |
| *utakula* | *utsola* | *utsola* | *hutapika* | *kumtsola* | *kumtsola* |
| *mtakula* | *mtsola* | *mtsola* | *hamukupika* | *kamtsola* | *kamtsola* |
| *atakula* | *atsola* | *atsola* | *hakupika* | *atsola* | *atsola* |
| *watakula* | *watsola* | *watsola* | *hawakupika* | *kawatsola* | *kawatsola* |

Tukichunguza data iliyomo katika Mfano Na. 8 hapo juu, tunabaini kwamba mofimu za ukanushi za wakati ujao, katika Kiswahili zinatofautiana na zile zinazojitokeza katika Kianzwani na Kimwali. Mathalani, mofimu {si} ya nafsi ya kwanza umoja katika Kiswahili inakuwa {ka} katika Kianzwani na Kimwali. Vilevile, mofimu za ukanushi za nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili wingi na nafsi ya tatu wingi katika Kiswahili, zinawakilishwa na mofimu {ha} ambapo katika Kianzwani na Kimwali mofimu hizo zinajitokeza kama {ka}. Aidha, katika kitenzi cha wakati ujao cha nafsi ya pili umoja katika Kiswahili mofimu ya ukanushi inakuwa {hu} ambapo katika Kianzwani na Kimwali mofimu hiyo inakuwa {ku}. Tofauti hizo za kimwonekano za mofimu za ukanushi baina ya Kiswahili, Kianzwani na Kimwali, zimesababishwa na mabadiliko ya konsonanti kama yalivyofafanuliwa katika kipengele cha 4.2 hapo juu. Hata hivyo, pamoja na mabadiliko hayo ruwaza za ujitokezaji wa mofimu za ukanushi katika lugha hizo unalingana. Data katika Mfano Na. 8 inadhihirisha kuwa ruwaza za mofimu za ukanushi katika nafsi ya kwanza umoja {si}, nafsi ya pili umoja {hu} na nafsi ya tatu umoja {ha} zimejitokeza kabla ya mofimu za wakati ujao. Wakati huohuo ruwaza za mofimu za ukanushi kwa vitenzi vya nafsi ya kwanza wingi {hu}, nafsi ya pili wingi {ha} na nafsi ya tatu wingi {ha}, zimejitokeza kabla ya mofimu za nafsi katika lugha hizo.

## 5.0 Hitimisho na Mapendekezo

Makala haya yameangazia na kujadili kuhusu ruwaza za mofimu za ukanushi katika Kianzwani, Kimwali na Kiswahili. Katika mjadala huo, tumeonesha jinsi mofimu hizo zinavyolingana na kutofautiana baina ya lugha hizo. Katika ulinganishi huo tumebaini kwamba, ruwaza za mofimu za ukanushi katika lugha hizo zinalingana ingawa baadhi zimetofautiana. Tofauti pekee iliyobainika ni ile ya mpishano wa konsonanti kama ambavyo imefafanuliwa katika makala haya. Mathalani, Kianzwani na Kimwali, mofimu ya ukanushi ya nafsi ya kwanza umoja katika wakati uliopo inawakilishwa na mofimu {si} kama ilivyo katika Kiswahili. Vilevile, mofimu ya ukanushi ya nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili umoja na wingi, nafsi ya tatu umoja na wingi katika Kianzwani na Kimwali zote zinawakilishwa na mofimu {ta, ka na kwa}. Katika Kiswahili mofimu hizohizo zinawakilishwa na {hu na ha} mtawalia kama tulivyokwisha kuzibainisha. Aidha, mofimu za ukanushi katika vitenzi vya wakati uliopita katika Kianzwani na Kimwali zinajitokeza kama {tsa, ka na kwa} katika nafsi ya kwanza hadi ya tatu umoja na wingi. Kwa upande wa Kiswahili, mofimu hizo zinajibainisha kama {si, hu na ha} katika nfsi zote umoja na wingi. Vilevile, tumebaini kwamba mofimu za ukanushi katika vitenzi vya wakati ujao vya Kianzwani na Kimwali zinajibainisha kwa mofimu {ka, ku na a} ambapo katika Kiswahili mofimu hizo zinajitokeza kama {si, ha, na hu} katika nafsi ya kwanza hadi ya tatu umoja na wingi.

Kuhusiana na tofauti ya baadhi ya mofimu za ukanushi zilizojitokeza katika lugha hizo, katika makala haya tumebaini kwamba, kuna sababu ambazo zimeukilia

tofauti hizo zitokee. Sababu mojawapo ni kwamba mabadiliko hayo yamechanuzwa na athari za kimazingira na kitamaduni zinazowakabili wazungumzaji wa lugha husika. Zaidi ya hayo umbali wa kijiografia baina ya lugha hizo, umechangia mabadiliko na mpishano wa sauti katika lugha zao. Kwa mfano, mofimu za ukanushi {si na ha} katika Kiswahili zimetofautiana na zile za Kianzwani na Kimwali ambazo ni {tsa na ka}. Hii inadhihirisha kwamba sauti [s na h] katika Kiswahili, Kianzwani na Kimwali zinatumia sauti [ts na k]. Hivyo, katika hali kama hiyo kulingana na isimu historia na linganishi, sauti hizo zinachukuliwa kama ni za aina moja. Hii inatokana na ukweli kwamba, sauti hizo zinarejeana kimnasaba kwa sababu zina upatanifu wa kiumbo licha ya tofauti inayojitokeza. Kwa mnasaba huo, Kianzwani, Kimwali na Kiswahili ni lugha zenye asili moja na hivyo huenda lugha hizo zimetokana na mame-lugha moja. Hivyo, tunapendekeza kufanyika utafiti zaidi katika lugha za asili nchini Komoro ili kubaini ruwaza za kufanana na kutofautiana kwake katika vipengele vingine mbalimbali vya kiisimu. Utafiti wa aina hiyo utatupatia mawanda mapana zaidi ambayo yatasaidia kutoa mahitimisho ya jumla kuhusu uhusiano wa lugha hizo na Kiswahili.

## Marejeleo


Anderson, S.R. (1992) *A-Morphous Morphology.*England: Cambridge University Press.

Aronoff, M. na Fudeman, K. (2011) *What is Morphology?* New York: John Wiley & Sons.

Asiimwe, C. (2019) *Ulinganishi wa Lugha za "Runyačitara".* Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapiswa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Bauer, L. (2003) *Introducing Linguistic Morphology.* Edinburgh: University Press.

Booij, G. (2005) *The Grammar of Words: An Introduction to Linguistic Morphology.* Oxford: Oxford University Press.

Chamanga, M. A. (2010) *Introduction à la Grammaire Structurale du Comorien le shiNgazidja.* Moroni: KomEDIT.

Chamanga, M. A. (2017) *Introduction à la Grammaire Structurale du Comorien le shiNdzuani* Moroni: KomEDIT.

Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1977) *Historia ya Kiswahili.* Nairobi: Oxford University Press.

Chomi, E.W. (2013) *Kitangulizi cha Mofolojia ya Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI.

Greenberg, J.H. (1966) *Language Universals with Special Reference to Feature Hierarchies.* The Hague: Mouton.

Habwe, J. na Katanja, P. (2012) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Hartman, R. (1972) *Dictionary of Language and Linguistics.* London: Routledge.

Haspelmath, M. (2002) *Understanding Morphology.* Oxford: Oxford University Press.

Katamba, F. (2017) *Morphology.* London: Routledge.

Kihore, Y.M, Massamba D. P. naMsanjila, Y. P. (2012) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: TUKI.

Kipacha, A. (2003) *Lahaja za Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Massamba, D.P.B. (2004) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B. (2007) *Kiswahili Origins and the Bantu Divergence-Convergence Theory.* Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B. (2017) *Historia ya Kiswahili: Mtazamo Mpya 100KK hadi 2000BK*. Dar es Salaam: Kiswahili Development Limited.

Nurse, D. (1989) *Is Comorian Swahili? Being an Examination of the Diachronic Relationship between Comorian and Coastal Swahili*. Paris: Editions Recherche sur les Civilisations.

Omar, A.S. (1985) *A Phonological Analysis of Shi-Ngazija*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Marealle, I.B. (1978) "Dhana ya Mofu, Mofimu na Alomofu". Katika *MULIKA,* Juz. 13.

Matinde, R.S. (2012) *Dafina ya Lugha, Isimu na Nadharia*. Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Matthews, P.H. (2014) *The Concise Oxford Dictionary of Linguistics.* Oxford: Oxford University Press.

Mgullu, R.S. (1999) *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Omar, A.S. (1985) "A Phonological Analysis of Shi-Ngazija". Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Palmer, F.R. (1988) *Morphology: A Study of the Relation between Meaning and Form.* Cambridge: Cambridge University Press.

Rotland, D. (1982). *Morphology: The Study of Structure.* Cambridge: Cambridge University Press.

Spencer, A na Zwicky, A.M. (Eds.). (2003) *The Handbook of Morphology.*England: Blackwell Publishing.

Stump, G.T. (2001) *Inflectional Morphology: A Theory of Paradigm Structure.* Cambridge: Cambridge University Press.

Trommer, J. (2017) *The Morphology and Phonology of Exponence.* Oxford: Oxford University Press.

Wesana-Chomi, E (2017). *Kitangulizi cha Muundo Viambajengo wa Sentensi za Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI.